WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Umuhimu wa Agizo la Ufundi Na. 1 la 2021 katika kuongeza uzalishaji wa mashamba ya watu binafsi na ya Serikali

Na

Dkt. Ezekiel E. Mwakalukwa

Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki

14 Novemba, 2021

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Maliasili na Utalii
AGIZO LA KIUFUNDI Na 1 LA 2021
UZALISHAJI WENYE
UBORA NA TIJA
Idara ya Misitu na Nyuki
Agosti, 2021

Technical order

- **MAMBO YANAYOTAKIWA KUZINGATIWA ILI KUPATA MALIGHAFI YENYE UBORA.**

- **KUZINGATIA TARATIBU ZA KUPANDA NA KUHUDUMIA MASHAMBA YA MITI**

1. KUOANISHA SPISHI NA MAHALI ZINAPOSTAHILI KUPANDWA

- Hakikisha kuwa kila aina ya spishi inapandwa katika maeneo sahihi ili iweze kupona, kustawi vyema na iwe na ubora na tija .

- Inapunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, shambulio la wadudu waharibifu na magonjwa.

2. KUCHANGANYA SPISHI ZA MITI

- Inapunguza athari za magonjwa, wadudu waharibifu, mabadiliko ya tabia nchi na ya kiuchumi.
- Inaongeza uhakika wa soko kwa kuwa na mazao mchanganyiko.
- Angalau **aina nne** tofauti za miti

3. MBEGU NA VIPANDIKIZI VINGINE

- Hakikisha mbegu na vipandikizi bora ndivyo **vinavyotumika** kwa ajili ya ustawishaji wa mashamba yenye ubora na tija.

4. VITALU VYA MICHE YA MITI

- **Kitalu cha miche** ni sehemu ambapo mimea inazalishwa na kukuzwa hadi kimo kinachotakiwa.

- Kuhakikisha kunakuwepo na uzalishaji wa **miche bora**, itakayopona na kustawi kwa haraka ipandwapo shambani.

5. UANZISHAJI WA MASHAMBA YA MITI

5. UANZISHAJI WA MASHAMBA YA MITI

- **Unajumuisha:** maandalizi ya mahali itakapopandwa miti, kuchimba mashimo, kuweka nafasi kati ya mashimo na kupanda.
- **Lengo ni** kuhakikisha kupona kwa miche kunakuwa kwa hali ya juu na ukuaji wa haraka ipandwapo shambani

6. UTUNZAJI WA MASHAMBA YA MITI

- Matunzo ya shamba **baada ya kupandwa** yanahitajika ili kuwa na msitu bora na wenye miti timilifu.
- Unatakiwa ufanyike vema na kwa wakati.
- **Unajumuisha: palizi** (Weeding), **upogoaji** (Pruning) na **upunguzaji idadi ya miti** iliyopandwa (Thinning).
- Lengo ni kupunguza ushindani wa unyevu ardhini, virutubisho, nafasi, pamoja na mwanga.

7. AFYA YA MISITU

- Tabianchi, wadudu waharibifu na magonjwa vinaweza **kuwa na athari kubwa** kwenye uhai wa mashamba ya miti.

- **Lengo la maelekezo haya ya kiufundi** ni kuhakikisha misitu inakingwa dhidi ya: moto, spishi vamizi, wadudu waharibifu na magonjwa ili kukuza tija na ubora.

8. UJENZI NA UTUNZAJI WA BARABARA ZA MSITUNI

- Kuna **aina kuu mbili** za barabara za msituni: *barabara ya kuingia* na *barabara-tawi*.
- ***Barabara ya kuingia*** inaunganisha msitu na barabara ya umma.
- ***Barabara-tawi*** ni kiungo kati ya eneo linalovunwa na barabara ya kuingia.

8. UJENZI NA UTUNZAJI WA BARABARA ZA MSITUNI

- **Lengo la maelekezo haya ya kiufundi** ni kutoa mtandao sanifu wa barabara ambao unathibitisha mwingilio kwenye eneo la utendaji, uwasilishaji wa vifaa vya kuanzisha msitu, ulinzi na utoaji wa mazao ya misitu unakuwa **kwa wakati** na kwa **gharama nafuu**.

9. UVUNAJI WA MISITU

- **Uvunaji wa misitu** ni kubadilisha miti kuwa mazao ya kutumika (k.m. magogo, nguzo, vinian.k) na hatimaye kupelekwa kwenye vituo vya kutumika.

- **Lengo la maelekezo** haya ni kufanya kazi hizo kwa ubora, uzalishaji mzuri, salama, wenye madhara madogo kwa mazingira ,na msitu utakaopandwa baadaye.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza!